# TNMC Habari

Toleo No. 0019

TOLEO MAALUMU

Marchi 2025

HALIUZWI

www.tnmc.go.tz

@tnmchabari

## Wauguzi, Wakunga 3281 Watunukiwa Vyeti, Leseni za Kitaaluma Jijini Dodoma.

Habari Uk. 01




Ukurasa 2



**TNMC Yaadhimisha Miaka 72 Na Watoto Wenye Ulemavu – Dodoma**

Ukurasa 4



**Wauguzi, Wakunga Endeleni Kubeba Dhamana Kama Serikali Ilivyowekeza**

Ukurasa 7



**Wakufunzi Wa Vyuo Vya Uuguzi Na Ukunga Watoa Maoni Kuboreshaji Sheria ya Baraza**

## Wizara Ya Afya Yawasilisha Bajeti Mwaka Wa Fedha 2024/25 Kwa Kamati ya Bunge

JARIDA MAALUMU
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

JARIDA MAALUMU BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlakaya Kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# TIMU YA WAHARIRI


**MWENYEKITI**

**Bi. Agnes Mtawa**

**MHARIRI**

**Mwakapiso Ndimmyake**

**WARATIBU**

**Irene Chilewa**

**Rose Mhando**

**MSANIFU JARIDA**

**Ezekiel Nyalusi**

# Wauguzi, Wakunga 3281 Wametunukiwa Vyeti, Leseni za Kitaaluma Jijini Dodoma.




Na. Mwandishi Wetu

Tarehe 21 Machi 2025, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania TNMC limeratibu Mahafali ya 13 ya kitaaluma yaliyofanyika Jijini Dodoma ambapo jumla ya wauguzi na wakunga 3281, wametunukiwa vyeti na leseni za kitaaluma.

Idadi hiyo ya Wataalamu inajumuisha ngazi ya Shahada ya Uuguzi yenye wataaluma 533, Shahada ya Ukunga 11, Shahada ya Uuguzi na Utaalamu wa Dawa za usingizi na ganzi 14, Stashahada ya Uuguzi na Ukunga 2,655 na Astashahada 68.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ambaye ndiye aliyekuwa Mgeni rasmi Prof. Lilian Msele, amewataka wanataaluma hao kuwa mfano wa kuigwa katika jamii na taaluma nyingine na kusema endapo



watawajibika mzuri katika suala zima la utoaji huduma, wachangia kuleta maendeleo katika taifa letu kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya hiyo.



***"Niwaase wauguzi wenzangu na wanataaluma wenzangu mkafanye yale mnayopaswa kufanya, Mkazingatie miiko na taratibu zote za kitaaluma,Sheria na miongozo mliyoelekezwa katika mafunzo na mpende kujiendeleza kitaaluma kwa kuwa tasnia hii inakua kilakukicha pasipokusahau mafunzo ya kujiendekeza kitaaluma mkiwa kazini yaani CPD"*** Alisema Prof. Msele

Naye Msajili wa Baraza hilo Bi. Agnes Mtawa, akizungumza na wauguzi hao kabla ya kula kiapo cha utii na uadilifu katika utumishi wao, amewakumbusha kuwa huduma za Uuguzi na Ukunga daima zinaongozwa na upendo na kama mwanataaluma hana upendo itamuwia vigumu sana kufanya kazi ya Uuguzi na Ukunga.

## Inaendelea......

***"Huduma zetu za uuguzi zinaongozwa na upendo, yaani lazima uwe na upendo na ndio maana tunawasha mshumaa kama taa ya upendo na utumishi bora maishani mwetu na leo kila mtu atasoma hiki kiapo, ndugu mgeni rasmi lakini pia hili ni tukio la kipee, kwa sababu kwa mara ya kwanza tunawasajili wauguzi wataalamu wa usingizi na ganzi tiba"*** Alisema Bi. Mtawa

Katika hatua nyingine msajili akasisitiza juu ya wauguzi na wakunga kuzingatia kanuni saba za kitaaluma.

***"Nataka niwaambie hizi kanuni ukizifahamu hutogombana na mtu yeyote mosi ni heshimu utu na Uhai, Pata idhini ya Mteja kabla ya kutoa Huduma, Dumisha Weledi na ujiendeleze kitaaluma, Uwe Mwaminifu na kutoa Huduma bila Upendeleo, Tunza siri za Mteja/ Mtu unaye Mhudumia, Timiza wajibu wako na kuwa tayari kuwajibika kwa Matendo yako na Shirikiana na watoa Huduma wengine na kufanya kazi kama timu."*** alisema Bi.Mtawa

Baraza la Uuguzi na Ukunga likiwa ni Mamlaka ya kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania, huandaa na kuendesha Mahafali ya kitaaluma kwa wauguzi na wakunga wahitimu wa vyuo mbalimbali vya ndani na nje ya nchi wanaofaulu Mtihani wa Baraza wenye lengo la kuhakiki umahiri katika taaluma hizo kabla ya mwanataaluma hajatunukiwa cheti cha usajili na leseni inayomruhusu kutoa huduma kwa jamii.



# TNMC Yaadhimisha Miaka 72 Na Watoto Wenye Ulemavu Mkoani Dodoma

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) 19 Machi 2025 limeadhimisha miaka 72 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1953, kwa kutembelea kituo cha Watoto wenye ulemavu kilichopo Mlali Wilayani Kongwa Mkoani Dodoma na kutoa msaada wa vyakula na vitu mbalimbali ikiwa ni utaratibu wake wa kurudisha shukrani kwa jamii na kusaidia watu wenye uhitaji.

Akizungumza wakati wa tukio hilo, kaimu Msajili TNMC Bi. Irene Chilewa amesema, katika kipindi cha miaka 72 Baraza limepata mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wauguzi na wakunga waliosajiliwa kufikia 53,000 katika ngazi mbalimbali



## Inaendelea...

za elimu ikiwa ni pamoja na uwepo wa wataalamu wa ngazi ya juu kabisa ya uzamivu PhD tofauti na miaka 72 iliyopita ambapo kulikuwa na wauguzi wachache na wengi wao walikuwa elimu ya cheti.

Ameongeza kuwa katika kipindi cha miaka 72 Baraza pia limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kusimamia maadili, miiko na miongozo ya kitaaluma katika utoaji huduma kwa jamii ili kuhakikisha wauguzi na wakunga



wanatoa huduma iliyobora na salama kwa jamii.

Bi. Irene ameyataja mafakio mengine kuwa ni pamoja na Ujenzi wa mfumo wa TEHAMA ambapo umekuwa chachu ya kurahisisha Mawasiliano na wanataaluma, utunzanji wa kielekroni wa kanzi data ya wauguzi na wakunga nchini pamoja na utambuzi wa wanataaluma wenye sifa ya kutoa huduma lakini pia ujenzi wa



Baraza Kibaha Mkoani Pwani na unaoendelea Jijini Dodoma.

***"katika kuadhimisha siku ya Baraza tumekuwa tukitoa misaada na vitu mbalimbali ikiwa ni sehemu ya kurudisha shukrani kwa jamii ambapo leo tumeleta mahitaji ya watoto yenye thamani ya Milioni Tano"*** amesema Bi. Irene

Naye Padri. Gaudence Aikaruwa, ambaye ni Mkurugenzi wa kituo hicho pamoja na kutaja changamoto wanazokumbanazo katika malezi ya watoto hao amelishukuru Baraza kwa misaada hiyo.

***"Kituo kinawatoto zaidi ya 40 wanaolelewa mahali hapa, huu msaada utatusaidia sana Tunashukuru na Mungu awabariki"*** amesema Fr. Gaudence

Nao baadhi ya wazazi wa watoto wenye ulemavu wametoa shukrani zao kwa Baraza kwa kutoa msaada huo huku wakitoa rai kwa watanzania wenye Watoto wenye ulemavu kutowafungia ndani badala yake wawapeleka katika vituo maalumu ili Watoto hao waweze pata haki zao za kimsingi ikiwa ni pamoja na elimu.

# Wauguzi, Wakunga Endeleeni Kubeba Dhamana Kama Serikali Ilivyowekeza -Mhe. Festo Dugange

Wauguzi, Wakunga na Watoa huduma za Afya kwa ujumla, wameagizwa kuendelea kubeba dhamana ya kuwapatia huduma bora Watanzania kama ambavyo Serikali ya awamu ya Sita ikiongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, inavyowekeza katika sekta ya Afya hapa nchini.

Hayo yamebainishwa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia masuala ya Afya Dkt. Festo Dugange, wakati akimwakilisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Mohamed Mchengerwa, katika ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa mwaka wa Wauguzi Viongozi Machi 26, 2025 Jijini Dodoma.

***"Ninawaelekeza Wauguzi Viongozi wa ngazi zote kuimarisha usimamizi wa utoaji wa huduma***




***bora ili wananchi wote wapate huduma bora na kwa usawa, tunatambua kuwa wauguzi wanafanya kazi nzuri sana, japo kuna baadhi yenu wachache wanaharibu sifa nzuri ya wauguzi kwa kufanya makosa mbalimbali yanayoweza kuepukwa,"*** amesema Dkt. Dugange.

Ameongeza kuwa kuwa katika ngazi ya Msingi pekee Serikali imewekeza jumla ya shilingi Trilioni 1.3 katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake sambamba na kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za Afya ya msingi.

Awali akimkaribisha mgeni rasmi, Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe, ambaye pia ndiye Mganga Mkuu wa Serikali, amepongeza ushiriki wa wauguzi katika mapambano ya magonjwa ya mlipuko husussani katika kuudhibiti ugonjwa wa Marburg ulikuwa umeibuka nchini

***"Tunapozungumzia wauguzi na wakunga ni rasilimali watu ambayo inafikia asilimia 60 ya wataalamu wote wa sekta ya Afya na majukumu mnayofanya yanafikia asilimia 80, huduma zote haziwezi kuboreka bila kuwa na rasilimali watu, inahitajika kuwa na watu wenye uwezo, weledi na ujuzi kama ninyi,"*** amesema Dkt. Magembe.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi na Ukunga Bi. Ziada Sellah ameishukuru Serikali kwa kuendelea kuboresha mambo mbalimbali ya kada hizo kwani hali ya sasa siyo sawa na miaka 10 iliyopita.

Naye Msajili wa TNMC Bi.Agnes Mtawa, akitoa salamu za shukrani kwa mgeni rasmi wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa mwaka wa wauguzi viongozi, Amesema TNMC itajitahidi kupunguza malalamiko yote yanayohusu muuguzi na mkunga kwa kusimamia vyema taaluma hiyo hapa nchini.

***"Ukizingatia uwekezaji wa Serikali katika upande wa Sekta ya Afya ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa mazingira ya utoaji huduma sasa malalamiko madogo madogo juu ya wauguzi na wakunga yanakwenda kuisha kitakachobaki ni kupongezwa tu"*** alisema Bi.Mtawa





# TNMC Yawafunda Watarajali Kabla Ya Kuanza Mafunzo Kwa Vitendo.



Na. Mwandishi Wetu

Watarajali zaidi ya 30 wamekutana Jijini Dodoma kwa lengo la kupata semina elekezi kabla ya kuanza mafunzo kwa vitendo katika maeneo mbalimbali ya kutolea huduma za Afya hapa nchini.

Semina hiyo iliyoandaliwa na Baraza la Uuguzi na ukunga na kuratibiwa na Kurugenzi ya Maadili, Usajili na leseni, imelenga kuwajengea uwezo wakutoa huduma katika vituo vyao vya mafunzo kwa kuzingatia kanuni, Sheria na miongozo ya taaluma ya Uuguzi na Ukunga hapa nchini.

Akizungumza na watarajali hao Msajili wa Baraza la Uuguzi na ukunga hapa Nchini Bi. Agnes Mtawa, amewakumbusha watarajali hao kuzingatia taratibu za kiuuguzi na Ukunga sambamba na kuwataka kufanya tafiti katika kada zao.



***"Sasa mmeshatoka vyuoni mnakwenda kuhudumia jamii nendeni mkahudumie jamii huku mkifanya tafiti za kutosha katika kada ya Uuguzi na Ukunga hatutegemei ninyi kukaa nyuma nyuma mmeandaliwa, mmeiva sasa nendeni mkafanye kazi"***- Bi. Mtawa.

Bi. Mtawa, ameongeza kwa kuwataka watarajali kuhakikisha wanakuwa na matumizi bora ya vifaa vyao vya mawasiliano sambamba na mitandao ya kijamii, huku akiwasisitiza kwenda kujifunza kwa vitendo.

Naye Mkurugenzi wa usajili, Leseni na Maadili TNMC Bi. Jane Mazigo, amewasisitiza watarajali hao kuhakikisha wanazingatia miongozo, uvaaji sare, na kanuni saba za maadili ya taaluma hiyo wakati wote wa utoaji huduma lakini pia kuhudhuria katika vituo vyao vya kazi kwa siku zote zilizopangwa na Baraza bila ya kukosa ili kuhakikisha wanapata mafunzo kwa ufasaha hivyo kuwa na weledi wakutosha katika taaluma ya Uuguzi na Ukunga.





# Wizara Ya Afya Yawasilisha Utekelezaji Bajeti Mwaka Wa Fedha 2024/25 Kwa Kamati ya Bunge



Na. Mwandishi Wetu

Katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Afya imeainisha vipaumbele vilivyozingatia uboreshaji wa utoaji wa huduma za Afya nchini ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa, kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za Afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi taifa ili kurahisha upatikanaji wa huduma hizo kwa wananchi.

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama, amesema hayo leo Machi 19, 2025 wakati akiwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/25 mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ikiongozwa na Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Bernadetha Mushashu.

"***Pia, Wizara imeimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za Afya nchini, Afya ya uzazi, Mama na Mtoto, upatikanaji na uendelezaji wa wataalamu katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi, huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi,***" amesema Waziri Mhagama.

Aidha, Waziri Mhagama amesema, katika kipindi cha utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2024/25 jumla ya akina mama wajawazito 1,846,540 walihudhuria kliniki ambapo kati yao, 1,744,980 sawa asilimia 94.5 walifanya mahudhurio manne ikilinganishwa na asilimia 91 katika kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita.

Waziri Mhagama amesema Wizara inaendelea kudhibiti kuingia nchini kwa magonjwa hatari yanayoambukiza ikiwemo ebola, marburg, mafua ya ndege, UVIKO-19, homa ya manjano pamoja na homa ya nyani (M-Pox) katika mipaka ambapo kipindi cha Julai 2024 hadi Februari 2025 jumla ya wasafiri 1,175,710 waliingia nchini na kufanyiwa uchunguzi wa awali.

Waziri Mhagama ametoa wito kwa wananchi kuendelee kujiunga na mifumo mbalimbali ya bima ya Afya ili kupata huduma za Afya bila kikwazo cha fedha, kwani hadi sasa asilimia 15 tu ya Watanzania wamejiunga na Mifumo ya Bima za Afya huku asilimia 85 ikiwa nje ya mfumo wa Bima ya Afya.



# Wakufunzi Wa Vyuo Vya Uuguzi Na Ukunga Watoa Maoni Kuboreshaji Sheria ya Baraza




Na. Ezekiel Nyalusi

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania TNMC kwa uratibu wa kitengo cha huduma za Sheria mnamo Machi 07 2025, liliendesha kikao maalumu na wakufunzi wawakilishi wa vyuo vya uuguzi na ukunga vilivyopo Mkoani Dodoma.

Kikao hicho kilikuwa na lengo la kupokea maoni ya uboreshaji wa Sheria ya Uuguzi na ukunga nchini Na. 1, ya mwaka 2010 ikiwa ni mwendelezo wa kukutana na makundi mbalimbali kupokea maoni kabla kuiwasilisha Bungeni kwa ajili ya marekebisho ili iendane na wakati.

Vyuo vilivyoshiriki ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) SJUT, KONDOA SON, DECOHAS, MIREMBE pamoja Chuo cha MVUMI.

Kabla ya kuanza kutoa maoni, Wajumbe walipitia vifungu vyote vya Sheria hiyo kisha wakatoa mapendekezo yao kwa ajili ya maboresho ikiwa ni pamoja na kupendekeza kuingizwa kwa vifungu vipya vitakavyokidhi matakwa ya Sheria kwa wakati uliopo.

Aidha, maoni mengine yalilenga kuboresha mazingira ya utoaji mafunzo ya taaluma ya Uuguzi na Ukunga katika Vyuo Vikuu na vya kati nchini Tanzania.

Awali wakufunzi hao walielezwa kwamba Ofisi ya Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania mara baada ya kuboresha Sheria itaanza mchakato wa kuboresha kanuni nne zinazosimamia utoaji huduma za Uuguzi ambazo zitaathiriwa na maboresho ya Sheria hii ya Mwaka 2010.

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania TNMC lipo katika hatua ya kukusanya maoni juu ya uboreshwaji wa Sheria namba moja ya mwaka 2010 kwa lengo kuhakikisha jamii inapata huduma zilizo bora na salama kwa kuisimamia vyema taaluma ya Uuguzi na Ukunga hapa nchini.



# Wadau Wakutana Kujadili Mtaala wa Kozi za Uuguzi,Ukunga Ngazi Ya Uzamili




**Na. Mwandishi Wetu**

**Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) Tarehe 17 Machi, 2025 limeratibu kikao kazi cha kupitia Mtaala wa mafunzo ya kozi za Uuguzi na Ukunga ngazi ya Shahada ya Uzamili.**

**Kikao kilichofanyika Jijini Dodoma, kinajumuisha wadau mbalimbali wa Kada za Uuguzi na Ukunga ambao ni Wakufunzi wa vyuo vikuu, wauguzi na wakunga wabobezi katika maeneo ya kutolea huduma (Clinical Nursing and Midwifery Experts), uongozi wa ECSACONM, wataalamu kutoka ECSA Regions, Baraza la Madaktari na Wizara ya Afya.**

**Baraza lipo katika kupitia na kuunganisha mtaala wa ECSACONM Fellowship ili kuupa ithibati kwa ajili ya kuanza kutumika hapa nchini.**

**Baraza la Uuguzi na Ukunga ni Mamlaka ya Kisheria inayosimamia wanataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria namba moja ya Mwaka 2010 (The Nursing and Midwifery Act, 2010) na Kanuni zake ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

# AINA YA MAFUNZO YA CPD NA MGAWANYO WA ALAMA

## 1 MAFUNZO AMBAYO YANAPATIKANA ENEO LA KAZI (NON-ACCREDITED CPD)

Mafunzo haya ni yale ambayo mtaaluma anayapata kila siku eneo lake la kazi na yanapangwa na wataaluma wenyewe yakilenga kuboresha hali ya utoaji wa huduma na huduma kwa ujumla. Yanachukua asilimia 50 sawa na alama 30 ambapo mtaaluma atatakiwa kupata alama 10 kwa mwaka

## 2 MAFUNZO YALIYORATIBWA NA KUPATA ITIBATHI ( ACCREDITED CPD)

Mafunzo haya yameandaliwa na wadau mbalimbali kuanzia eneo la utoaji wa huduma na wanaosimamia miradi. Yanachukua asilimia 30 sawa na alama 18 ambapo mtaaluma atatakiwa kupata alama 6 kwa mwaka

## 3 MAFUNZO YANAYOPATIKANA KWA NJIA YA MTANDAO ( ONLINE CPD)

Mafunzo haya yanatolewa kupitia mtandao – mtaalamu anatakiwa kusoma maeneo yanayoongeza umahiri katika utoaji wa huduma. Yanachukua asilimia 20 sawa na alama 12 ambapo mtaaluma atatakiwa kupata alama 4 kwa mwaka. Mtaaluma atasoma kupitia application ya WCEA ***(https://engagement.wcea.education/tnmc)*** na National e-leaning platform - ya Wizara ya Afya

### JEDWALI : MGAWANYO WA ALAMA ZA MAFUNZO (CPD AWARDING POINTS)

| SN | AINA YA CPD | MGAWANYO WA ALAMA % | ALAMA KWA MWAKA | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2023 | 2024 | 2025 |
| 1 | NON-ACCREDITED CPD | 50% | 10 | 10 | 10 |
| 2 | ACCREDITED CPD | 30% | 6 | 6 | 6 |
| 3 | ONLINE CPD | 20% | 4 | 4 | 4 |
| | JUMLA | 100% | 20% | 20% | 20% |

*NB: Jumla ya alama za mafunzo anazotakiwa kupata mtaaluma ili kuhuisha Leseni yake ni 60 ndani ya miaka mitatu (2023 hadi 2025)*

# MAOMBI YA MTIHANI WA USAJILI NA LESENI

**Dirisha lipo wazi kuanzia 12.04.2025 hadi 12.05. 2025**

**MUOMBAJI ANATAKIWA KUZINGATIA TARATIBU ZOTE ZA MAOMBI KAMA IFUATAVYO : -**

- **Kufaulu Mtihani wa kufuzu Mafunzo kwa ngazi husika *(qualifying examination)***
- **Kuwa na namba ya utambulisho *(Indexing Number)* kwa mujibu wa kifungu cha 14 (1) cha kanuni za mafunzo**
- **Kuweka picha sahihi *(Passport Size 45mmX35mm) background iwe ya Lightblue,***
- **Kujaza majina sahihi yanayoendana na vyeti vya kumaliza Elimu ya Sekondari**
- **Kufanya malipo na kuchagua kituo sahihi cha Mtihani kwa wakati.**

# TAARIFA YA TANZIA

**Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepokea kwa Masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mwezi Machi, 2025, baada ya kumaliza kazi ya hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao Mahali pema Peponi AMENI.**



**JINA:** MWAJUMA IDDI ISMAIL
**KITUO:** ZAHANATI YA KIBAHA
**MKOA:** PWANI



**JINA:** BERNAD JOHN MNENWA
**KITUO:** MWANANYAMALA RRH
**MKOA:** PWANI

# JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu: 0736 00 60 60**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA